

KUMB: PPR/17 - 05/1

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA MAFUTA AINA YA PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 3 MEI 2017

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini. Bei hizi zitaanza kutumika kuanzia **Jumatano, Tarehe 3 Mei 2017**. Pamoja na kutambua bei kikomo za bidhaa mbalimbali za petroli nchi nzima, ni muhimu kuzingatia yafuatayo:-

- (a) Bei za jumla na rejareja kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua ikilinganishwa na toleo lililopita la tarehe 5 Aprili 2017. Kwa mwezi Mei 2017, bei za rejareja kwa Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa zimepungua kama ifuatavyo: TZS 31/lita sawa na asilimia 1.48, TZS 80/lita sawa na asilimia 4.18 na TZS 16/lita sawa na asilimia 0.88, sawia. Vilevile, kwa kulinganisha na toleo la mwezi uliopita, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli, Dizeli na Mafuta ya Taa nazo zimepungua kama ifuatavyo: TZS 30.50/lita sawa na asilimia 1.57. TZS 80.42/lita sawa na asilimia 4.43 na TZS 16.31/lita sawa na asilimia 0.93, sawia. Kupungua kwa bei za mafuta kwenye soko la ndani, kwa kiasi kikubwa kumetokana na kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia na kuongezeka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, sarafu ambayo hutumika kununulia mafuta.
- (b) Bei za jumla na za rejareja kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Tanga, nazo zimepungua isipokuwa Mafuta ya Taa ambapo bei hazijabadilika kwa sababu hakuna mzigo mpya wa Mafuta ya Taa uliopokelewa katika mwezi wa Aprili 2017 kuititia bandari ya Tanga. Katika toleo hili, bei za rejareja kwa Petroli na Dizeli zimepungua kama ifuatavyo: TZS 127/lita sawa na asilimia 6.10 na TZS 86/lita sawa na asilimia 4.40, sawia. Aidha, bei za jumla kwa mafuta ya Petroli na Dizeli kwa mkoa wa Tanga nazo zimepungua kwa TZS 127.44/lita sawa na asilimia 6.44 na Dizeli TZS 85.57/lita sawa na asilimia 4.67, sawia. Kupungua kwa bei za mafuta katika soko la ndani, kwa kiasi kikubwa kumetokana na kupungua kwa bei za mafuta katika soko la dunia na gharama za usafirishaji (*BPS Premium*) pamoja na kuongezeka kwa thamani ya Shilingi dhidi ya Dola ya Marekani, fedha ambayo hutumika kununulia mafuta. Bei za mkoa wa Tanga zimepungua zaidi ukilinganisha na za Dar es salaam kutoptana na ukweli kuwa hakukuwa na mzigo mpya wa mafuta uliopokelewa katika mwezi Machi 2017 kuititia bandari ya Tanga.
- (c) Mamlaka inapenda kuukumbusha umma kwamba bei kikomo za mafuta kwa eneo husika, zinapatikana vile vile kuititia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kuititia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- (d) Kwa mujibu wa Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta. Taarifa hizi zina lengo la kuwasaidia wadau kufanya maamuzi stahiki kuhusu manunuzi ya bidhaa za mafuta.

- (e) **Kampuni za mafuta zipo huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani mradi tu bei hizo ziwe chini ya bei kikomo (price cap)** kama ilivyokokotolewa na *fomula* iliyopitishwa na EWURA na ambayo ilichapishwa katika **Gazeti la Serikali Na. 70/2016 la mwezi Februari 2016.**
- (f) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana na yakionesa bei ya mafuta, punguzo, vivutio vya biashara au promosheni zinazotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei ndogo zaidi ili kushamirisha ushindani. **Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutokeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- (g) Wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi ya malipo inayoonesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hiyo ya malipo itatumika kama kidhibiti cha mnunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya ama kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yenyewe kiwango cha ubora kisichofaa.

A: BEI ZA REJAREJA

Mji	Bei Kikomo		
	Petroli (Shs/Lita)	Dizeli (Shs/Lita)	Mafuta ya Taa (Shs/Lita)
Dar es Salaam	2,027	1,844	1,842
Arusha	2,111	1,928	1,926
Arumeru (Usa West)	2,111	1,928	1,926
Karatu	2,129	1,947	1,944
Monduli	2,116	1,934	1,931
Monduli-Makuyuni	2,121	1,938	1,936
Ngorongoro (Loliondo)	2,202	2,020	2,017
Kibaha	2,031	1,849	1,847
Bagamoyo	2,038	1,856	1,853
Kisarawe	2,034	1,852	1,849
Mkuranga	2,037	1,854	1,852
Rufiji	2,055	1,872	1,870
Dodoma	2,086	1,903	1,901
Bahi	2,093	1,910	1,908
Chemba	2,112	1,929	1,927
Kondoa	2,118	1,936	1,933
Kongwa	2,083	1,900	1,898
Mpwapwa	2,087	1,904	1,902
Iringa	2,091	1,908	1,906
Kilolo	2,095	1,913	1,910
Mufindi (Mafinga)	2,101	1,918	1,916

Njombe	2,119	1,936	1,934
Ludewa	2,157	1,975	1,972
Makete	2,150	1,967	1,965
Wanging'ombe (Igwachanya)	2,117	1,934	1,932
Bukoba	2,242	2,059	2,057
Biharamulo	2,216	2,034	2,031
Karagwe (Kayanga)	2,258	2,076	2,073
Kyerwa (Ruberwa)	2,264	2,081	2,079
Muleba	2,242	2,059	2,057
Ngara	2,207	2,025	2,022
Misenyi	2,250	2,068	2,065
Geita	2,192	2,009	2,007
Bukombe	2,181	1,998	1,996
Chato	2,213	2,030	2,028
Mbogwe	2,230	2,047	2,045
Nyang'hwale	2,207	2,024	2,022
Kigoma	2,258	2,075	2,073
Uvinza (Lugufu)	2,270	2,087	2,085
Buhigwe	2,247	2,064	2,062
Kakonko	2,215	2,032	2,030
Kasulu	2,244	2,061	2,059
Kibondo	2,222	2,040	2,037
Moshi	2,101	1,918	1,916
Hai (Bomang'ombe)	2,104	1,921	1,919
Mwanga	2,094	1,911	1,909
Rombo (Mkuu)	2,121	1,939	1,936
Same	2,087	1,904	1,902
Siha (Sanya Juu)	2,107	1,925	1,922
Lindi	2,086	1,903	1,901
Lindi-Mtama	2,104	1,921	1,919
Kilwa Masoko	2,061	1,878	1,876
Liwale	2,107	1,924	1,922
Nachingwea	2,115	1,932	1,930
Ruangwa	2,116	1,934	1,932
Babati	2,149	1,967	1,964
Hanang (Katesh)	2,160	1,977	1,975
Kiteto (Kibaya)	2,160	1,978	1,975
Mbulu	2,162	1,979	1,977
Simanjiro (Orkasumet)	2,181	1,999	1,996
Musoma	2,205	2,023	2,020
Musoma Vijijini (Busekela)	2,246	2,063	2,061
Rorya (Ingirijuu)	2,214	2,031	2,029
Rorya (Shirati)	2,249	2,066	2,064
Bunda	2,196	2,014	2,011
Butiama	2,202	2,019	2,017

Serengeti (Mugumu)	2,251	2,068	2,066
Tarime	2,216	2,034	2,031
Mbeya	2,134	1,951	1,949
Chunya	2,143	1,961	1,958
Chunya (Makongolosi)	2,157	1,975	1,972
Ileje	2,147	1,964	1,962
Kyela	2,150	1,967	1,965
Mbarali (Rujewa)	2,118	1,935	1,933
Mbozi (Vwawa)	2,143	1,961	1,958
Momba (Chitete)	2,152	1,969	1,967
Rungwe (Tukuyu)	2,143	1,960	1,958
Morogoro	2,052	1,869	1,867
Mikumi	2,068	1,885	1,883
Kilombero (Ifakara)	2,090	1,907	1,905
Kilombero (Mlimba)	2,112	1,930	1,927
Kilombero (Mngeta)	2,101	1,919	1,916
Ulanga (Mahenge)	2,100	1,918	1,915
Malinyi	2,110	1,928	1,926
Kilosa	2,070	1,888	1,885
Gairo	2,070	1,888	1,885
Mvomero (Wami Sokoine)	2,062	1,880	1,877
Turian	2,077	1,894	1,892
Mtvara	2,099	1,917	1,914
Nanyumbu (Mangaka)	2,148	1,965	1,963
Masasi	2,125	1,942	1,940
Newala	2,131	1,949	1,946
Tandahimba	2,124	1,942	1,939
Mwanza	2,177	1,994	1,992
Kwimba	2,213	2,030	2,028
Magu	2,185	2,002	2,000
Misungwi	2,182	2,000	1,997
Sengerema	2,209	2,027	2,024
Ukerewe	2,236	2,054	2,051
Sumbawanga	2,199	2,017	2,014
Kalambo (Matai)	2,192	2,009	2,007
Nkasi (Namanyele)	2,213	2,030	2,028
Katavi (Mpanda)	2,234	2,052	2,049
Mlele (Inyonga)	2,213	2,030	2,028
Songea	2,150	1,968	1,965
Mbinga	2,184	2,001	1,999
Namtumbo	2,179	1,997	1,994
Nyasa (Mbamba Bay)	2,186	2,003	2,001
Tunduru	2,209	2,026	2,024
Shinyanga	2,156	1,973	1,971
Kahama	2,169	1,987	1,984

Kishapu	2,184	2,001	1,999
Simiyu (Bariadi)	2,197	2,014	2,012
Busega (Nyashimo)	2,190	2,007	2,005
Itilima (Lagangabilili)	2,200	2,017	2,015
Maswa	2,188	2,006	2,003
Meatu (Mwanhuzi)	2,195	2,013	2,010
Singida	2,117	1,935	1,932
Iramba	2,130	1,947	1,945
Manyoni	2,102	1,919	1,917
Ikungi	2,113	1,930	1,928
Mkalama (Nduguti)	2,142	1,959	1,957
Tabora	2,181	1,998	1,996
Igunga	2,135	1,952	1,950
Kaliua	2,199	2,016	2,014
Ulyankulu	2,193	2,010	2,008
Nzega	2,145	1,963	1,960
Sikonge	2,193	2,010	2,008
Urambo	2,194	2,011	2,009
Tanga	1,963	1,858	1,664
Handeni	1,983	1,879	1,684
Kilindi	1,998	1,894	1,699
Korogwe	1,975	1,870	1,676
Lushoto	1,984	1,880	1,685
Mkinga (Maramba)	1,970	1,865	1,671
Muheza	1,967	1,863	1,669
Pangani	1,969	1,865	1,670

B: BEI ZA JUMLA

Bei za Jumla - DSM	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,915.95	1,733.48	1,730.96

Bei za Jumla-TANGA	Petroli (Sh/L)	Dizeli (Sh/L)	Mafuta ya Taa (Sh/L)
Bei Kikomo	1,851.60	1,747.28	1,552.80

Felix Ngamlagosi

**MKURUGENZI MKUU
EWURA**